**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/135/EZ/2024/06**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000112**

**KATI YA**

**ANTHONY AUGUSTI LYIMO ............................................................ MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) ........................... MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 02 mwezi Januari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 02 mwezi Januari 2025, kwa madai kwamba Mlalamikiwa aamriwe kusitisha kukata fedha pindi Mlalamikaji anaponunua umeme.

Mlalamikaji akiwakilishwa na Bi. Mary Lucas Mbuya anaeleza kwamba maofisa wa Mlalamikiwa walifika eneo lake kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa miundombinu, na baada ya uchunguzi huo, walitoa ripoti ya uchunguzi ambayo inaonyesha kwamba kuna upotevu wa umeme wenye thamani ya kiasi cha TZS 774,850.50. Mlalamikaji anaeleza kwamba aliingiziwa madai hayo kama ankara ambayo malipo yake yatafanyika kila atakapo kuwa ananunua umeme.

Mlalamikaji anaendelea kueleza kwamba aliwasilisha malalamiko yake ofisi ya Mlalamikiwa ili waweze kuondoa ankara hiyo kwa sababu yeye hajasababisha upotevu wa umeme bali ni tatizo la Mlalamikiwa kuweka dira ya umeme ambayo haina viwango. Mlalamikaji anaendelea kueleza zaidi kwamba alifuatilia kwa muda mrefu utatuzi wa suala hili lakini alikosa msaada kutoka ofisi ya Mlalamikiwa na aliamua kuwasilisha malalamiko yake kwa Mamlaka (EWURA).

Baada ya kupokea malalamiko tarehe 8 Julai 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Mnamo tarehe 09 Mei 2024, Mlalamikiwa alileta utetezi wake na kukiri kupokea malalamiko ya Mlalamikaji na kueleza kwamba Mlalamikaji anapaswa kulipa ankara ambayo amewekewa kwenye dira yake kwa maana ni halali na imetokana na matumizi ya umeme ambao ameutumia Mlalamikiwa anaendelea kueleza kwamba Mlalamikaji anapaswa kuthibitisha kuwa ankara aliyowekewa kuwa si halali ili maombi yake yatekelezwe kama alivyoomba kwenye fomu ya malalamiko.

Kikao cha usuluhishi baina ya pande mbili kilifanyika mnamo tarehe 13 Mei 2024 na tarehe 17 Juni 2024, na mwisho wa kikao, Mlalamikiwa aliomba kupewa muda wa kuzungumza na Mlalamikaji nje ya Mamlaka ili kufikia muafaka wa kile kinacholalamikiwa.

Mnamo tarehe 5 Disemba 2024 Mlalamikaji aliwasilisha ujumbe mfupi wa maneno ukionyesha kuwa amemalizana na Malalamikiwa na anaondoa shauri lake.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yaondolewe na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 02 mwezi Januari 2025.

..................................
**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**